

Inachukua

dakika 2 tu.

Tanzania Sea Rescue ni shirika la kujitolea la uokoaji, majini. Washiriki wetu mahiri wanaojitolea wanategemea kujikusanya haraka an KUNGOA Nanga ya Mashua ya Uokoji ndani ya dakika 30 baada ya kupokea tarifa ya kuomba Msaada. Kama huwezi kubaki salama majini mwenyewe, waweza funikwa na mawimbi ndani ya dakika 2 na mashua yetu itakua imechelewa sana.

Je nini kingine kinachukua dakika 2 tu? Jipange kabla nanma ya kuwa salama, endapo utakumbana na ugumu wowote usiotegemewa:

BAKI UMEELEA Hakikisha kwamba, mashua yako ina vifaa ndani vitakavyosaidia kuelea, na uwe unafahamu namna ya kuvitumia. Tunashauri kwamba kila mashua iwe inabeba "lifejacket" kwa ajili ya kila aliepanda ndani. Katika dharura, hata kushikilia chupa kubwa tupu ama kushikilia kwenye kitu chochote kinachoweza kuelea vizuri, ni bora kuliko kukaa bure.

ONEKANA Mwokoaji hataweza kukuokoa kama hakuoni. Jitahidi kukaa karibu na mashua, pia walio kwenye maji washikane pamoja. Ni rahisi Zaidi kutambua kitu kikubwa kuliko mtu mmoja majini. Distress flairs zitakusaidia kuwafahamisha ama kutoa ishara kwa wengine kuwa unahitaji msaada. Nyakati za usiku ni vigumu kwa mwokoaji kukupata isipokua kama una chombo chenye mwanga mkali.

JIFUNZE KUTOA TAARIFA YA Katika maeneo ya karibu na nchi kavu, njia nzuri ya kuomba masaada ni kutumia Radio call ama simu ya kiganjani. Kitengo cha Uokoaji Majini (MRCC) ni kitengo cha kupokea na kuratibu shughuli za uokoaji majini. Watakiagiza chombo kinachopatika na kinachofaa kuja kukusaidia, na inawezekana ikawa ni mashua ya Tanzania Sea Rescue. Kwa hali ya dharua, MRCC wanapatika kupitia namba:

0800 110 019 / 0800 110 020 / 0767 886 295 / VHF - Channel 16

Photo: with kind permission from Renee Blundon seaunseen.com



TANZANIA SEA RESCUE
Saving lives in Tanzanian waterways



Tanzania Sea Rescue ni taasisi isoyoyote ya malengo ya Kifaida, inayoendesha kwa namna ya watu kujitolea iliyo na malengo ya kuokoa maisha ya watu katika maji ya Tanzania. Shughuli zake zinaendesha kwa michango ya hiari kutoka kwa watu binafsi, na kwa udhamini wa taasisi za kibashara zinazoguswa na usalama baharini kwa Watanzania wote. Makampuni haya yanajumuisha.